

KUMB: PPR/16 - 11/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 2 NOVEMBA 2016**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Novemba 2016**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Oktoba 2016. Kwa Mwezi Novemba 2016, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kama ifuatavyo: TZS 33/lita sawa na asilimia 1.80, TZS 21/lita sawa na asilimia 1.25 na TZS 11/lita sawa na asilimia 0.64 sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimeongezeka kama ifuatavyo: TZS 33/lita sawa na asilimia 1.91, TZS 21/lita sawa na asilimia 1.33 na TZS 11/lita sawa na asilimia 0.68. Kupanda huku kwa bei za mafuta kwenye soko la ndani, kwa kiasi kikubwa kumetokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia
- (b) Bei za jumla na za rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Tanga, zimebadilika ikilinganishwa na toleo la bei za mafuta hayo lililopita la tarehe 05 Oktoba 2016. Kwa Mafuta ya Taa hakuna mabadiliko ya bei, hii imetokana na kutopokewa shehena mpya ya Mafuta ya Taa katika bandari ya Tanga kwa mwezi wa Oktoba 2016. Katika toleo hili, bei ya rejareja kwa Petroli imeongezeka kwa TZS 64/lita sawa na asilimia 3.61 na Dizeli imepungua kwa TZS 12/lita sawa na asilimia 0.71. Aidha, kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli imeongezeka kwa TZS 64/lita sawa na asilimia 3.84 na Dizeli imepungua kwa TZS 12/lita sawa na asilimia 0.76 .
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (e) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 70/2016 la Mwezi Februari 2016**.
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na

kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

- (g) Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	1,860	1,720	1,669
Arusha	1,944	1,804	1,753
Arumeru (Usa West)	1,944	1,804	1,753
Karatu	1,962	1,822	1,771
Monduli	1,950	1,809	1,758
Monduli-Makuyuni	1,954	1,814	1,763
Ngorongoro (Loliondo)	2,036	1,895	1,844
Kibaha	1,865	1,725	1,673
Bagamoyo	1,871	1,731	1,680
Kisarawe	1,867	1,727	1,676
Mkuranga	1,870	1,730	1,679
Rufiji	1,888	1,748	1,696
Dodoma	1,919	1,779	1,727
Bahi	1,926	1,786	1,735
Chemba	1,945	1,805	1,754
Kondoa	1,952	1,812	1,760
Kongwa	1,916	1,776	1,725
Mpwapwa	1,920	1,780	1,729
Iringa	1,924	1,784	1,733
Kilolo	1,929	1,789	1,737
Mufindi (Mafinga)	1,934	1,794	1,743
Njombe	1,952	1,812	1,761
Ludewa	1,990	1,850	1,799
Makete	1,983	1,843	1,792
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,950	1,810	1,759
Bukoba	2,075	1,935	1,884
Biharamulo	2,050	1,909	1,858
Karagwe (Kayanga)	2,092	1,951	1,900
Kyerwa (Ruberwa)	2,097	1,957	1,906

Muleba	2,075	1,935	1,884
Ngara	2,041	1,901	1,849
Misenyi	2,084	1,944	1,892
Geita	2,025	1,885	1,834
Bukombe	2,014	1,874	1,823
Chato	2,046	1,906	1,855
Mbogwe	2,063	1,923	1,872
Nyang'hwale	2,040	1,900	1,849
Kigoma	2,091	1,951	1,900
Uvinza (Lugufu)	2,103	1,963	1,912
Buhigwe	2,080	1,940	1,889
Kakonko	2,048	1,908	1,857
Kasulu	2,077	1,937	1,886
Kibondo	2,055	1,915	1,864
Moshi	1,934	1,794	1,742
Hai (Bomang'ombe)	1,937	1,797	1,746
Mwanga	1,927	1,787	1,736
Rombo (Mkuu)	1,955	1,815	1,763
Same	1,920	1,780	1,729
Siha (Sanya Juu)	1,940	1,800	1,749
Lindi	1,919	1,779	1,728
Lindi-Mtama	1,937	1,797	1,746
Kilwa Masoko	1,894	1,754	1,703
Liwale	1,940	1,800	1,748
Nachingwea	1,948	1,808	1,757
Ruangwa	1,950	1,810	1,758
Babati	1,982	1,842	1,791
Hanang (Katesh)	1,993	1,853	1,801
Kiteto (Kibaya)	1,993	1,853	1,802
Mbulu	1,995	1,855	1,804
Simanjiro (Orkasumet)	2,014	1,874	1,823
Musoma	2,038	1,898	1,847
Musoma Vijijini (Busekela)	2,079	1,939	1,888
Rorya (Ingirijuu)	2,047	1,907	1,856
Rorya (Shirati)	2,082	1,942	1,890
Bunda	2,030	1,889	1,838
Butiama	2,035	1,895	1,844
Serengeti (Mugumu)	2,084	1,944	1,892
Tarime	2,049	1,909	1,858
Mbeya	1,967	1,827	1,776
Chunya	1,977	1,837	1,785
Chunya (Makongolosi)	1,991	1,851	1,799
Ileje	1,980	1,840	1,789
Kyela	1,983	1,843	1,791
Mbarali (Rujewa)	1,951	1,811	1,760

Mbozi (Vwawa)	1,976	1,836	1,785
Momba (Chitete)	1,985	1,845	1,794
Rungwe (Tukuyu)	1,976	1,836	1,785
Morogoro	1,885	1,745	1,694
Mikumi	1,901	1,761	1,709
Kilombero (Ifakara)	1,923	1,783	1,732
Kilombero (Mlimba)	1,945	1,805	1,754
Kilombero (Mngeta)	1,935	1,794	1,743
Ulanga (Mahenge)	1,934	1,794	1,742
Malinyi	1,944	1,804	1,752
Kilosa	1,904	1,764	1,712
Gairo	1,904	1,764	1,712
Mvomero (Wami Sokoine)	1,896	1,756	1,704
Turian	1,910	1,770	1,719
Mtwara	1,933	1,792	1,741
Nanyumbu (Mangaka)	1,981	1,841	1,790
Masaki	1,958	1,818	1,767
Newala	1,965	1,824	1,773
Tandahimba	1,958	1,818	1,766
Mwanza	2,010	1,870	1,819
Kwimba	2,046	1,906	1,855
Magu	2,018	1,878	1,827
Misungwi	2,016	1,876	1,824
Sengerema	2,042	1,902	1,851
Ukerewe	2,069	1,929	1,878
Sumbawanga	2,033	1,893	1,841
Kalambo (Matai)	2,025	1,885	1,834
Nkasi (Namanyele)	2,046	1,906	1,855
Katavi (Mpanda)	2,068	1,928	1,876
Mlele (Inyonga)	2,046	1,906	1,855
Songea	1,983	1,843	1,792
Mbinga	2,017	1,877	1,825
Namtumbo	2,013	1,873	1,821
Nyasa (Mbamba Bay)	2,019	1,879	1,828
Tunduru	2,042	1,902	1,851
Shinyanga	1,989	1,849	1,797
Kahama	2,002	1,862	1,811
Kishapu	2,017	1,877	1,826
Simiyu (Bariadi)	2,030	1,890	1,839
Busega (Nyashimo)	2,023	1,883	1,832
Itilima (Lagangabilili)	2,033	1,893	1,842
Maswa	2,022	1,882	1,830
Meatu (Mwanhuzi)	2,029	1,889	1,837
Singida	1,951	1,811	1,759
Iramba	1,963	1,823	1,771

Manyoni	1,935	1,795	1,744
Ikungi	1,946	1,806	1,755
Mkalama (Nduguti)	1,975	1,835	1,784
Tabora	2,014	1,874	1,823
Igunga	1,968	1,828	1,777
Kaliua	2,032	1,892	1,841
Ulyankulu	2,026	1,886	1,835
Nzega	1,979	1,839	1,787
Sikonge	2,026	1,886	1,834
Urambo	2,027	1,887	1,836
Tanga	1,846	1,691	1,659
Handeni	1,867	1,712	1,680
Kilindi	1,882	1,727	1,695
Korogwe	1,858	1,703	1,671
Lushoto	1,868	1,713	1,681
Mkinga (Maramba)	1,853	1,698	1,666
Muheza	1,851	1,696	1,664
Pangani	1,853	1,698	1,666

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,752.26	1,612.16	1,560.84

Bei za Jumla-TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,738.36	1,583.09	1,551.08

Felix Ngamlagosi

**MKURUGENZI MKUU
EWURA**